# OFISI YA RAISI – TAMISEMI

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO

**SHULE YA SEKONDARI SELEBU**
**S.L.P 177,**
**MAZOMBE**
Simu 0758354570/0629321254

Kumb Na:KDC/ SELSS/JOIN/2021/01

Jina la Mwanafunzi ……………………………………………...............

SHULE ALIYOSOMA...........................................................................

**YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SELEBU WILAYA YA KILOLO MKOA WA IRINGA- MWAKA 2021**

### 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** Katika shule hii mwaka **2021**,Shule ya Sekondari **SELEBU** Ipo umbali wa km **110** kutoka makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo.

Mhula wa kwanza wa masomo unaanza Tarehe **11/01/2021**, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia Tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni Tarehe **16/01/2021**.

### 2.0 SARE ZA SHULE

a) **WAVULANA**:

(i) Suruali 2 rangi **NYEUSI** mshono: chini upana inch 18 wenye mkunjo,yenye marinda mawili juu ya mifuko ya mbele na mfuko wa nyuma usiwe na zipu.Mkanda wa suruali upana inch 2 wenye Ruksi)

(ii) Mashati 2 meupe (tetroni)mikono **MIFUPI.**

(iii) Viatu jozi 2 vyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu.

(iv) Soksi jozi 2 au zaidi rangi **NYEUSI**

(v) Sweta rangi ya **BLUU** yenye( V) upande wa mbele isiyo na maandishi/mchoro.

(vi) Mkanda mweusi usiwe na nembo yoyote.

(vii) Sare za michezo: bukta moja na fulana yake, raba na TRAKISUTI rangi **BLUE YENYE MKANDA MWEUPE(MTELEZO)**

**b) WASICHANA:**

i) Sketi 2 ndefu Zenye kufunika soksi rangi ya **NYEUSI** Mshono: marinda 8 ya kupanga yenye mfuko upande wa kushoto, mkanda inch 2 (zingatia rangi ya kitambaa kihoambatanishwa )
ii) Shati (blauzi) 2 nyeupe (tetroni) mikono **MIFUPI**
iii) Viatu jozi mbili vyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu.
iv) Soksi ndefu jozi 2 au zaidi rangi **NYEUPE**
v) Sweta rangi ya **BLUE** yenye (V) upande wa mbele lisilo na maandishi/mchoro
vi) Hijabu(Nyeupe).
vii) Sare za michezo: Bukta moja flana yake raba na TRAKISUTI moja rangi **ya blue YENYE MKANDA MWEUPE (MTELEZO)**

**NB.Zingatia rangi na mshono wa sare za shule.**

**3.0 VIFAA VYA KUJIFUNZIA:**

i) Daftari **16** kaunta books kwaya 2
ii) Kalamu **10** na penseli **05**
iii) Mkebe **1** wa hesabu
iv) Begi la kubebea daftari
v) Rula

**4.0 MAHITAJI YA KIBINADAMU**

i) **MATIBABU**: mwanafunzi aje na kadi ya C H F (kadi ya Bima ya afya) kwa ajili ya Matibabu, ikumbukwe kuwa jukumu la matibabu ni la mzazi.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolea na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:-

a) Heshima kwa viongozi ,wazazi,wafanya kazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(preparation).
d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
i) Kutunza mali za umma.

**5.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE:**

a) Wizi.
b) uasherati na ushoga.
c) Ubakaji.
d) ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji Bangi, Cocaine, Mirungi na Kubeli.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/Kupata Mimba.
i) Kuoa au Kuolewa.
j) Kutoa mimba.
k) Kugoma,Kuchochea na Kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) Kuwa na simu ya mkononi.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

...............................

**FERDINAND.M.MWANYIKA**
**MKUU WA SHULE**

HEADMASTER
SELEBU SECONDARY SCHOOL
IRINGA

**KILOLO DISTRICT COUNCIL**
**SELEBU SECONDARY SCHOOL**
**P.O BOX 177, MAZOMBE.**

# FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by Medical Officer in respect of all form one entrants

Full Name ..............................................................................................................

Age ............years. Sex ...........................................................................................

Blood count (red and white) ......................................................................................

Stool examination ...................................................................................................

Urine analysis .........................................................................................................

Syphilis test ...........................................................................................................

Eye test ..................................................................................................................

T.B test ..................................................................................................................

Ears .......................................................................................................................

Chest .....................................................................................................................

Spleen ....................................................................................................................

Abdomen .................................................................................................................

UPT ........................................................................................................................

ADDITION INFORMATION eg physical or chronicle of family disease,etc ..........................

.................................................................................................................................

I certify that the above is fit to pursue studies.

Signature ............................................

Designation ...........................................

Section ................................................

Date ....................................................

NOTE: Pupils, You must bring the complete form when you come to school.Pupils without certificate of physical fitness will not be accepted.

FERDINAND.M.MWANYIKA
HEADMASTER

HEADMASTER
SELEBU SECONDARY SCHOOL
IRINGA